JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

"Kilimani" Iringa Road,
S.L.P. 1175,
41101 DODOMA,
Barua Pepe: rbcdodoma@pccb.go.tz.
TANZANIA.

www.pccb.go.tz

DODOMA – DESEMBA 18, 2020

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI
VIWANJA VYAREJESHWA KWA WALIODHULUMIWA

Ndugu Wanahabari,
Tunakutana kuwapatia taarifa mbalimbali za utendaji wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma kwa lengo la kuelimisha umma kwamba rushwa ni adui wa haki na hailipi.

Kwanza, Ufuatiliaji wetu wa miradi ya maendeleo umewezesha kampuni ya Leostart Engineering ya Jijini DSM kurejesha Serikalini shilingi milioni arobaini na tano laki saba sitini mia tano sitini na moja (45,760,561/=) ikiwa ni sehemu ya fedha alizolipwa kinyume na taratibu wakati wa utekelezaji wa mradi wa maji wa Kijiji cha Mlongia wilayani Chemba. Mtakumbuka siku za nyuma tuliwahi kuwataarifu kuhusu ufuatiliaji wetu wa mradi huo na ukaguzi maalum uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulionyesha kwamba Mkandarasi wa mradi huo wenye thamani ya shilingi 579,323,000/= ulioanza mwaka 2013 na kukamilika 2014 alilipwa fedha zaidi ya kazi zilizofanyika na hivyo kutakiwa kuzirejesha.

Pili, Leo tunampatia Bw. Dismas Kweka, Mfanyabiashara na Mkazi wa Nkhuhungu Jijini Dodoma, shilingi milioni tisa na laki saba (9,700,000/=) ambapo ufuatiliaji wetu umewezesha kuzirejesha kutoka kwa Bw. Richard Mwambeje. Awali, Bw. Kweka aliuziwa kiwanja Na. 18 Kitalu B kilichopo Mbwanga Jijini Dodoma kinyume na utaratibu kwani kiwanja hicho kilitolewa na mwananchi mmoja kama sadaka kwa Jumuiya ya Uamsho wa Wakristo Tanzania (UWATA). Bw. Mwambeje ambaye alikuwa Katibu wa UWATA alipokea shilingi milioni kumi na tisa (19,000,000/=) baada ya kutengeneza mkataba wa kughushi hivyo anapaswa kurejesha kiasi kilichosalia huku hatua nyingine za kiuchunguzi zikiendelea. Awali Bw. Kweka alisharudishiwa shilingi milioni mbili. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, umiliki wa kiwanja hicho umerejeshwa kwa UWATA.

Tatu, leo pia tunamrejeshea Bi. Grace Matona Kusevya ambaye ni Muuguzi Mstaafu na Mkazi wa Jijini Dodoma shilingi milioni nane laki sita na elfu tisini (8,690,000/=) zikiwa ni fedha alizokuwa anaidai JW Micro Credit ya Jijini Dodoma toka mwaka 2016. Ufuatiliaji wa TAKUKURU umeonyesha kuwa Bi. Kusevya aliipatia kampuni hiyo shilingi milioni ishirini

(20,000,000/=) kwa ahadi ya kulipwa fedha hizo na faida lakini si tu kwamba hakulipwa faida yoyote bali pia hata fedha yenyewe alilipwa sehemu tu hadi tulipoingilia kati na kuwezesha kulipwa kiasi kilichosalia.

Nne, kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, tumeweza kuwasaidia wananchi watano kupata viwanja vyao ambavyo aidha walidhulumiwa au walipatiwa eneo ambalo tayari lilikuwa na mmiliki mwingine. Wananchi hao wamepatiwa viwanja namba 180 kitalu ZF eneo la Michese; namba 48 Kitalu F eneo la Kikuyu Kusini; namba 20 Kitalu B eneo la Mlimwa Kaskazini; namba 131 Kitalu F eneo la Kikuyu Kusini; na namba 451 na 453 Kitalu CC eneo la Mkalama.

Pia tumemrejeshea mwananchi mmoja shilingi milioni moja na elfu sitini (1,060,000/=) alizotapeliwa na Bw. Job Mosses Makasi (43), mkazi wa Ipagala Jijini Dodoma, ambaye alimwahidi kumwuzia kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 1250 kilichopo eneo la Mlimwa C Jijini Dodoma kwa kiasi cha shilingi milioni kumi na tatu (13,000,000/=) lakini 'Dalali' huyo akakata mawasiliano tangu Agosti, 2020 baada ya kupokea malipo ya awali, hadi tulipomtia nguvuni.

Tano, TAKUKURU imewezesha kuokoa na itarejesha kwa Uhamiaji SACCOS eneo lenye ukubwa wa hekari tano lililopo Ihumwa Jijini Dodoma. Ufuatilaji wetu umeonyesha kwamba mwaka 2017 Bw. Ezekiel Mchemwa, Mkazi wa Nzuguni Jijini Dodoma, aliuza eneo hilo kwa Uhamiaji SACCOS kwa shilingi milioni sitini na tano (65,000,000/=) lakini baadaye akauza tena eneo hilo kwa watu wengine. Wakati wa zoezi la urasimishaji mwaka huu, ilibainika kwamba eneo hilo lina wamiliki wengine na ndipo tukafuatilia na kuwezesha eneo kurejeshwa kwa SACCOS hiyo. Uchunguzi wa kijinai bado unaendelea.

Sita, Jamhuri imeshinda mashauri matatu yaliyohusu mashtaka ya kuomba na kupokea rushwa kinyume na kifungu cha 15(1)a cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

- **Kwanza**, Mahakama ya Hakimu Mkazi Dodoma imetoa uamuzi wa shauri la jinai namba 145/2019 na kumhukumu Bw. Abdulhakim Abbas Kabuga (27) ambaye alikuwa ni 'BVR Operator' wa NIDA kulipa faini ya shilingi laki tano au kifungo cha miaka mitatu. Alifikishwa mahakamani kwa kupokea hongo ya shilingi elfu thelathini ili amsaidie mtoa taarifa kupata kitambulisho cha uraia mapema.

- **Pili**, Mahakama hiyo pia imemhukumu Mtendaji wa Kijiji cha Mapanga wilayani Chamwino Bw. Daudi David Tengeneza kulipa faini ya shilingi laki tano au kifungo cha miaka mitatu baada ya kuridhishwa na ushahidi katika shauri la jinai namba 12/2019 kwa mashtaka ya kushawishi rushwa ya shilingi laki tatu na kupokea laki moja kutoka kwa Mfugaji ili amruhusu kuingiza mifugo kijijini bila kuwa na barua ya kuhamisha mifugo.

- **Tatu**, Mahakama ya wilaya Kondoa imemhukumu Mtendaji wa Kata ya Thawi Bw. Hashim Ally Mohamed (42) katika shauri la jinai namba 26/2020 kulipa faini ya

shilingi laki tatu au kifungo cha miaka miwili baada ya kuridhishwa na ushahidi kwamba alishawishi rushwa ya shilingi 175,000/= na kupokea 80,000/= ili asimchukulie hatua mzazi ambaye hakumpeleka binti yake sekondari baada ya kufaulu.

Mwisho tunapenda kuwakumbusha wakazi wa Mkoa na hasa Jiji la Dodoma kuwa makini sana wanapotaka kununua ardhi. Kuna wimbi la madalali matapeli na hata watumishi wasio waaminifu hivyo ni muhimu sana kujiridhisha kupitia vyombo stahiki kuhusu uhalali wa eneo unalotaka kununua kabla ya kufanya malipo yoyote.

Tunaendelea kuwataka wananchi kutupa taarifa za vitendo vya rushwa nasi tutazifanyia kazi kwa weledi na uharaka.

Imetolewa na:

Sosthenes Kibwengo
Mkuu wa TAKUKURU (M) Dodoma